

336/1

LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI

Paper 1

JULAI 2026

2HRS

INTERNAL MOCK EXAMINATION

UGANDA CERTIFICATE OF EDUCATION

Karatasi Ya Kwanza

(Uandishi Wa Insha Na Ufupisho)

Saa mbili

MAAGIZO KWA WATAHINIWA:

- *Karatasi hii ina sehemu mbili: A na B.*
- *Jibu maswali mawili kwa jumla ukichagua moja katika kila sehemu.*
- *Majibu yaandikwe kwa kijitabu ulichopewa.*

SEHEMU A
UANDISHI WA INSHA

Ama

1. Katika jamii yako umegundua kuwa baadhi ya wasichana na wanawake wamenyimwa haki zao za msingi kama masomo na kufanya kazi kwa sababu jamii inaamini shughuli hizo ni za wavulana pekee. Mkuu wa jamii amekuagiza umwandikie Afisa wa Wilaya ukieleza hali hiyo na kupendekeza njia za kuhimiza usawa na dhima ya mwanamke. Andika utakayo wasilisha **(Tumia maneno 200-220)**

Au

2. Katika kijiji cha Songa Mbele paliishi makabila mawili kwa muda mrefu. Hata hivyo baada ya uchaguzi wa viongozi wa kijiji, baadhi ya watu walianza ubaguzi, kudharau na kujitenga kwa misingi ya kikabila. Hali hii ilisababisha kuvunjika kwa ushirikiano na kupungua kwa shughuli za maendeleo. Wewe kama mwanakijiji aliyehudhuria mkutano huo wa kutafuta suluhisho na kudumisha amani, eleza yaliyojadiliwa. **(Tumia maneno 200-250)**

SEHEMU B

UFUPISHO

3. *Kumekuwa na mkutano kuhusu magonjwa ambapo mwenyekiti Muwanguzi ameeleza mengi kuhusu vyanzo vya magonjwa uliweza kuhudhuria mkutano huo na kuelewa kila hoja liloelezwa. Iandike tena kwa ufupi ukitumia maneno 80.*

Afya ni jambo muhimu katika maisha ya mwanadamu kwa sababu humwezesha mtu kushiriki kikamilifu katika shughuli za kila siku. Hata hivyo, katika jamii nyingi, idadi ya watu wanaouguua magonjwa mbalimbali imeendelea kuongezeka. Hali hii imechangiwa na mambo kadhaa yanayohusiana na mwenendo wa watu pamoja na mazingira wanamoishi. Ingawa wahudumu wa afya wameendelea kutoa elimu kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa, bado baadhi ya watu hawazingatii maelekezo yanayotolewa.

Mazingira anamoishi mtu yana mchango mkubwa katika hali yake ya afya. Maeneo yenye taka nyingi, maji yaliyotuma na uchafu mwingine huwa mazalia ya wadudu wanaoweza kusababisha magonjwa. Vilevile, matumizi ya maji kutoka sehemu zisizo salama bila kuyatibu huongeza uwezekano wa watu kupata matatizo mbalimbali ya kiafya. Wakati mwingine, shughuli za kibinadamu kama utupaji ovyo wa taka na ukosefu wa mifumo bora ya majitaka huzidisha tatizo hilo.

Mbali na mazingira, tabia za watu binafsi pia zinaweza kuhatarisha afya zao. Watu wengine hawazingatii usafi wa mwili na huendelea na shughuli zao bila kufuata kanuni rahisi za kujikinga na magonjwa. Aidha, ulaji wa vyakula visivyo na virutubisho vya kutosha au vilivyotayarishwa katika mazingira yasiyo safi huweza kuathiri afya ya mtu. Matumizi ya vileo kupita kiasi na uvutaji wa sigara ni mienendo mingine inayoweza kusababisha matatizo makubwa mwilini.

Katika jamii nyingine, watu hupuuza umuhimu wa kupata huduma za afya kwa wakati unaofaa. Baadhi yao huchelewa kwenda hospitalini wanapougua au hutumia dawa bila ushauri wa wataalamu. Wengine hukataa huduma muhimu za kinga kwa sababu ya imani potofu au taarifa zisizo sahihi. Kutokana na hali hii, magonjwa huendelea kuenea na kuleta athari kwa maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla.

Ili kupunguza tatizo la magonjwa, kila mtu anapaswa kuwajibika katika kulinda afya yake na ya wengine. Kuzingatia usafi, kufuata ushauri wa wataalamu wa afya na kubadilisha mienendo hatari ni hatua muhimu katika kujenga jamii yenye afya bora.

MWISHO